

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Check for updates

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 4, Issue 1, 2023

**Article Information**
Submitted: 10th October 2022
Accepted: 17th December 2022
Published: 21st February 2023

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Muia, S. T., Mutua, J., & Makoti, V. (2023). Mchango wa mandhari katika kusawirisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya ya Maisha Kitendawili. *Research Journal in African Languages*, 4(1). Retrieved from https://royalliteglobal.com/african-languages/article/view/1052

# Mchango wa mandhari katika kusawirisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*

**Shadrack Tete Muia, John Mutua, Vifu Makoti**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: shadracktete@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-2473-8539

**Abstract**
This article analyses the centrality of context in mediating the subject matter in John Habwe's novel Maisha Kitendawili (2000). It shows how, the writer carefully utilizes context to bring out his message and develop various stylistic devices in the novel. This article also examines how various contexts are used in conveying message in Maisha Kitendawili. Scenery is one of the aspect of stylistic devices. Stylistic devices are used by the writer to convey message to the reader in an interesting manner in the literary work. The aim of this paper is to examine how John Habwe has used scenery as an aspect of stylistic device in conveying his message to the society. This article also recognizes the contribution of other aspects of stylistic devices but will limit itself in revealing how scenery helps in conveying message to the reader of the novel; Maisha Kitendawili. So, the critics will show the sceneries used in the novel; Maisha Kitendawili. Moreover, the critic believes that by using John Habwe's novel he is able to show how different scenaries have enabled the author achieve his objective. This article is guided by realism theory which emphasizes that literature work should use real scenery that is familiar to the writer and reader so as to depict the real life situations. Findings of this research shows that the author of the novel, Maisha Kitendawili has used scenery as a pillar in conveying his message.

**Keywords:** content, context, mediation, style, scenery

© 2023 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

# Mchango wa mandhari katika kusawirisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*

**Shadrack Tete Muia, John Mutua, Vifu Makoti**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Correspondence: shadracktete@gmail.com
https://orcid.org/0000-0003-2473-8539

**Ikisiri**
Makala hii inalenga kuhakiki mandhari katika riwaya ya John Habwe; *Maisha Kitendawili* (2000). Lengo la makala ni kuchunguza na kubainisha jinsi ambavyo mwandishi John Habwe alivyotumia mandhari kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii. Pia wahakiki wanamadhumuni ya kubainisha jinsi mandhari mbalimbali yanavyomwezesha mwandishi kufikia lengo lake. Mandhari ni sehemu ya fani. Fani ndicho kipengele kinachomuwezesha mwandishi wa fasihi kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji kwa namna ya kuvutia. Lengo la makala ni kuchunguza na kubainisha jinsi ambavyo mwandishi John Habwe alivyotumia mbinu ya utunzi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii. Aidha, makala hii inatambua mchango wa vipengele vingine vya fani lakini itajikita katika kubainisha jinsi ujenzi bora wa mandhari unavyofanikisha uwasilishaji wa ujumbe kwa msomaji wa riwaya; *Maisha Kitendawili*. Kwa hivyo, mhakiki anabainisha mandhari kwenye riwaya, *Maisha Kitendawili*. Pia mhakiki anaamini kuwa kwa kutumia riwaya za John Habwe anaweza kubainisha jinsi mandhari mbalimbali yanavyomwezesha mwandishi kufikia lengo lake. Makala hii inaongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo husisitiza kuwa kazi ya fasihi itumie mandhari halisi ambayo si mageni kwa mwandishi na msomaji ili kuwasilisha ukweli wa maisha halisi. Matokeo ya uhakiki huu yamedhihirisha kuwa mwandishi wa riwaya, *Maisha Kitendawili* John Habwe ametumia mbinu ya mandhari kama uti wa mgongo kufanikisha ujumbe wake.

**Maneno Muhimu:** mandhari, ubunifu, ujumbe, upatanishi, uwasirisaji

**Public Interest Statement**
It cannot be gainsaid that setting is where and when the story takes place. Every story occurs in some time period at some geographical location(s). Setting can include topography, climate, and weather when these are integral to the story. The two key elements of a story's setting are the time and place in which the author situates their characters and plot. An effective setting will feed the reader's imagination, enabling them to visualise characters and their actions and help readers to understand the culture, society, and values that the story seeks to advance. As such, this article explores the centrality of context in mediating meaning in John Habwe's *Maisha Kitendawili*.

**Utangulizi**

Lengo la kila mwandishi wa kazi ya fasihi ni kufikisha ujumbe kwa wasomaji. kazi ya fasihi huathiriwa na mazingira anamoishi mwandishi. Huchota yale yanayotokea katika Maisha ya kila siku ya jamii yake. Kwa hivyo, mwandishi huandika juu ya yale yanayotokea katika hali halisi. Ujumbe huo unaweza kuwa na lengo la kuelimisha, kuonya, kutahadharisha, kuburudisha au baadhi ya malengo haya. Ujumbe huo ni kipengele muhimu katika fasihi na hususan iwapo mwandishi anataka kazi yake iwe faafu katika jamii yake. Kazi yake hulenga kuifahamisha jamii yake yale yaliyomo ndani mwao, yawe mazuri au mabaya. Kwa hivyo Ujumbe huo aghalabu unaweza kuakisi hali halisi ya jamii. Ili kuwasilisha ujumbe huo kikamilifu, inambidi mwandishi atume mbinu za kisanii mbalimbali. Mbinu hizi za kisanii hujumuisha jinsi masimulizi hutekelezwa kupitia kwa wahusika mbalimbali, mbinu za uandishi, mandhari na lugha. Kazi ya fasihi hutumia wahusika, mbinu za uandishi, Mandhari na lugha ili kufikia lengo la mwandishi. Jambo hili hufanya kazi ya mwandishi kuwa tofauti na mwandishi mwingine. Vile vile utofauti wa tanzu za fasihi huwaelekeza mwandishi kutumia fani zinazofaa mwandishi kutumia rani zinazofaa ili kuwasilisha Ujumbe wanaotaka.

Mandhari ni mbinu muhimu katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Mandhari hushirikiana na vipengele vingine vya fani ili kuwezesha ujumbe kuwasilishwa kwa msomaji kikamilifu. Kila jambo linalotendeka katika jamii hutendeka mahali fulani, yaani mandhari halisi na vivyo hivyo kazi za kifasihi nazo hufuata mkondo uo huo kwa sababu fasihi huchota katika mazingira ya mwandishi. Mwandishi wa fasihi anaweza kutumia mandhari halisi au mandhari ya kubuni. Mandhari yawe ya kubuni au halisi hushirikiana na ujumbe ili kazi ieleweke kwa urahisi. Jambo hili humfaidi msomaji na pia mwandishi wa kazi husika.

Makala hii inahusu uchanganuzi wa mandhari katika riwaya ya Maisha Kitendawili. Mwandishi huyu John Habwe ni Mwandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili hususan riwaya. Ametumia Mandhari kwa ufundi pevu wa kisanii katika riwaya ya Maisha Kitendawili. lengo la Makala ni kuchunguza na kubainisha jinsi ambavyo mwandishi John Habwe alivyotumia Mandhari kama kipengele cha utunzi ili kuwasilisha ujumbe wake kwa jamii. Mwandishi wa Makala hii hazingatii vipengele vyote vya fani bali anazingatia Mandhari na ujumbe. Kwa kuzingatia vipengele hivi, mhakiki ana imani kwamba anakuwa katika nafasi nzuri ya kudhihirisha mchango wa mandhari katika ufanikishaji wa ujumbe wa mwandishi kikamilifu.

**Nadharia ya Uhalisia**

Makala hii inaongozwa na nadharia ya uhalisia ili kushughulikia kipengele cha mandhari katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Katika makala hii, uhalisia unachukuliwa kama mtazamo unaoeleza kazi ya kifasihi ambazo huwasilisha uhalisia wa mambo kupitia ujumbe uliokusudiwa. Kulingana na Msokile (1993) kazi yoyote ya fasihi inatarajiwa kuonyesha mazingira halisi na itaje mambo yanayodhihirika katika jamii. Zaidi ya hayo, kazi hiyo itumie wahusika ambao wanaonyesha hali halisi ya jamii, wahusika hao wawe wa kawaida na wanaopatikana katika maisha halisi ya mwanadamu. Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007) uhalisia hujikita katika kutumia wahusika ambao wanaonekana katika hali halisi ya jamii. Pia, wahusika huendelezwa vile ambavyo hupatikana katika mandhari ya kawaida

wakati watunzi wanapoandika hadithi zao. Nadharia hii hueleza kuwa kazi ya mwandishi inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mandhari yake, mandhari katika kazi za fasihi yawe mandhari halisi. Kwa hivyo, makala hii inabainisha mandhari mbalimbali yaliyotumiwa katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* na kuonyesha mchango wa mandhari hayo katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi.

**Dhana ya Mandhari**

Fasihi hujengwa na vipengele mbalimbali vya fani ikiwemo matumizi pevu ya kipengele cha mandhari. Kipengele hiki ni muhimu katika uandishi wa fasihi na huwa kinachangia katika kujenga ujumbe wa mwandishi. Kwa hivyo, mandhari ni kipengele cha sanaa ambacho mwandishi wa fasihi hukitumia kuwasilisha ujumbe wake kwa msomaji.

Kipengele cha mandhari kimefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Tutaaangalia ufafanuzi wa wataalamu wawili. Njogu na Chimera (2008, p. 46) wanaeleza mandhari kama mazingira ya wahusika pamoja na matukio yao, mle mnamokaa wahusika hao na kushirikiana katika njia za kiuchumi. Wataalamu hawa wanahusisha mandhari na matukio ya kihistoria, kiutamaduni, kiwakati, kihali pamoja na maelezo ya kijiografia ambapo mwandishi hubuni katika uandishi wa hadithi yake.

Naye Wamitila (2008) anaeleza mandhari kama elementi ambayo humfichulia msomaji ni wapi na lini matukio fulani yalifanyika. Mandhari yanaweza kuwa na uhalisia au yawe hayana uhalisia bali ya kidhahania. Mandhari ya uhalisia yanahusu mahali ambamo au ambapo panapatikana katika dunia halisi, mfano mandhari ya msitu, chuoni, nyumbani, ofisini, mjini na maabadini. Mandhari ya kidhahania yanahusu mazingira yasiyo ya kawaida na mengi huonekana kupitia ndoto. Mfano wa mandhari ya kidhahania ni peponi, kuzimu na jahanamu.

Kwa hivyo, kutokana na fafanuzi za Njogu na Chimera na Wamitila tunaweza fasili kuwa mandhari ni sehemu, mahali, eneo au hata hali ambapo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itakapotendeka. Kazi ya fasihi ya fasihi yoyote ile, lazima iandamane na sehemu au mahali ambapo matukio hutokea. Mandhari yanahusishwana wahusika, ujumbe na mtindo uliotumika katika kazi ya fasihi.

Mandhari yana manufaa katika kazi ya fasihi kwa sababu zifuatazo. Mandhari huwezesha ujenzi wa migogoro katika kazi yoyote ya fasihi. Migogoro hii hutokea baina ya wahusika waliopo katika mandhari yale au waliopo katika mandhari tofauti. Migogoro hii ndiyo inayozua ujumbe wa mwandishi. Pia mandhari hutuwezesha kuhisi au kupata tajiriba ya yale mwandishi anayotaka kuwasilisha kwa wasomaji na jamii yake kwa jumla. Mwandishi anapotumia mandhari fulani huwa ametutoa ulimwengu wa kiubunifu hadi ulimwengu wa kiuhalisia. Msomaji wa fasihi huweza kuchora picha halisi zinazohusiana na kazi za mwandishi.

**Mandhari katika riwaya ya Maisha Kitendawili**

Pamedhihirika mandhari mbalimbali katika riwaya ya *Maisha kitendawili*, lakini tumeyaweka katika makundi mawili tu. Mandhari ya mahali na mandhari ya hali. Mwandishi John Habwe ametumia mandhari hayo katika kufanikisha ujumbe wake.

**Mandhari ya Mahali**

Mandhari ya mahali hueleza ni wapi tukio limetokea. Kila kisa katika fasihi huwa na sehemu tofauti na huwa na mandhari tofauti. Mahali pa pekee panaweza kutumiwa kutoa asili ya ujumbe mpya. Mandhari ya mahali yanaweza yakachukua dunia, nchi, jiji, mji, kijiji na kitongoji. Mandhari ya mahali katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* yamejitokeza pale ambapo mwandishi anaeleza wahusika wake. Ifuatayo ni mifano ya mandhari ya mahali iliyotumiwa na mwandishi wa *Maisha Kitendawili*.

**Mandhari ya Nyumbani**

Katika *Maisha Kitendawili* kuna mandhari ya nyumbani ambako wahusika mbalimbali waliishi.

Kwanza nyumbani kwa mhusika Papi. Kupitia mhusika Papi mwandishi anadhihirisha picha halisi ya nyumba yake, jinsi ilivyojengwa na kupambwa. Mwandishi anaeleza: Ilikuwa nyumba ya kifahari ambayo ilikuwa na ukumbi mkubwa wakuvutia. Sakafuni kulirembeshwa kwa zulia jekundu. Pia kulikuwa na viti vya bei ghali. Taa ya stima ilining'inia kwenye paa la nyumba. Ukutani picha ya Papi ilikuwa imetiwa upande wa matlai na upande mwingine wa ukuta kulikuwa na kabati refu lililotiwa mapambo likawa linavutia (uk.21).
Mandhari haya ya nyumbani kwa mhusika Papi yanadhihirisha ujumbe wa utabaka. Familia hii imo tabaka la matajiri kwani waliishi jumba la kifahari mno. Pia vitu vilivyopatikana katika nyumba ya mhusika Papi ni dhahiri kuwa vilikuwa vya bei ghali. Gari ambalo alimiliki lilikuwa la kifahari.

Pia mna mandhari ya nyumbani kwa Kasu na Yasmini. Wahusika hawa waliishi katika maskani duni. Chumba walichoishi mlangoni mlikuwa na pazia la chandarua iliyochanwa, ilikusanya rangi nyingi hadi kutambua rangi halisi ilikuwa vigumu. Kazi ambazo walizifanya hazikuwa na mapato mengi kwa kuwa waliuza makaa kwenye kibanda nje ya nyumba waliyoishi. Pesa walizopata kutokana na biashara hii ya kuuza makaa, hazikutosha kulipia nyumba kodi. Jambo hili lilisababisha Kasu na Yasmini kufanya ukahaba ili wapate pesa za kulipa kodi ya nyumba. Hili linadhihihirika kwa: "... Kasu na Yasmini hufanya nipe nikupe mpaka wakadunduliza ngwenje kulipa kodi. Wakati Fulani hulipa shilingi tano na wakamshtakia tajiri na kumwambia wanatarajia nyingine kutoka kwa wateja…uk. 26."

Mandhari haya ya nyumbani kwa Kasu na Yasmini yametumika na mwandishi kuwasilisha ujumbe wa utabaka. Wahusika hawa ni watabaka la chini (maskini). Wanaishi katika maskani duni na wanatafuta njia mbadala kujikimu kimaisha. Njia ambazo pia wanatumia kupata pesa wakati mwingine hazitoshelezi mahitaji yao ya kila siku kama kupata chakula na mavazi mazuri.

Mandhari ya nyumbani pia yanajitokeza kwa mhusika Mama Josii. Kupitia mhusika Kasu mwandishi anaonyesha picha halisi ya nyumbani kwa Mama Josii. Familia ya Mama Josii ilipitia hali ngumu ya maisha. Watoto wa Mama Josii walilala sakafuni ambapo palitiwa jivu. Zaidi ya hayo, watoto hao walitandikiwa karatasi ambazo walizitumia kama gondoro (uk.67). Taa iliyotumika katika familia hiyo ilikuwa ya kibatari. Nyumba pia ilikuwa inavuja maji paani na ukutani msimu wa mvua. Mvua inaponyesha maji yalilowa kila mahali kwenye nyumba yao. Kupatikana kwa chakula katika nyumba ya Mama Josii ilikuwa tabu. Mama Josii ndiye aliyekuwa tegemeo la pekee katika familia hiyo. Hili lilitokana na kuwa mumewe mgonjwa na hakuwa na uwezo wa kufanya kazi. Jukumu la kutunza familia liliachiwa Mama Josii pekee. Kwa hivyo, Mama Josii alijikakamua kulea watoto ambao walikuwa wengi pamoja na mumewe. Watoto wake Mama Josii, Agnes na Jane hawakuwa wanaenda shule licha ya wao kutimiza umri wa kuenda shule (uk.69). Kutojiunga na shule kulitokana na Mama Josii kukosa karo ya kuwapeleka shuleni. Mandhari haya yanadhihirisha familia iliyopitia hali ngumu ya maisha hivyo kudhihirisha ujumbe wa utabaka (tabaka la maskini).

Bila shaka, mandhari haya ya nyumbani yanadhihirisha uhalisia uliopo baina ya matabaka mbalimbali yaliyokuwa yakiishi katika jamii ya mwandishi. Mandhari haya ni halisi kwani yanadhihirika katika jamii halisi ya mhakiki. Nchi nyingi za Afrika zimegawika katika matabaka mawili. Tabaka la chini (maskini) na tabaka la juu (matajiri). Tabaka la chini (maskini) linaishi katika mandhari ya kutamausha kama mandhari yaliyoishi wahusika Kasu, Yasmini na Mama Josii. Tabaka hili kupata mahitaji muhimu ni changamoto na wakati mwingine hulazimika kufanya kinyume na maadili ya jamii ili kutimiza mahitaji muhimu kama kupata lishe, mavazi na pia karo ya shule. Tabaka la juu (matajiri) liliishi maisha ya starehe kwani linauwezo wa kutimiza mahitaji muhimu kama kupata lishe bora, malazi mazuri na matibabu mazuri. Tabaka hili linaishi katika mijengo ya kifahari ambayo imejengwa kwa gharama ghali, wanamiliki magari ya kifahari na wana walinzi wa mchana na usiku katika majumba yao.

**Mandhari ya Chuoni**

Mwandishi ametumia mandhari ya chuoni katika sehemu kadha wa kadha katika riwaya ya *Maisha*

*Kitendawili*. Jamii ya *Maisha Kitendawili* inachukulia swala la elimu kwa uzito, kwa kuwa kuna wale waliosoma hadi chuo kikuu kama Farida, Rose, Mary, Amos  na Juma. Wote wanadhihirisha uhodari wao katika elimu. Rose anafanya vizuri masomoni kiasi cha kupewa tuzo katika Chuo Kikuu cha Mzalendo. Mwandishi pia amedhihirisha jinsi sherehe ya kufuzu kwa mahafali chuoni Mzalendo ilivyoandaliwa katika uwanja wa chuo sehemu iliyojulikana Biko Square (uk.73). Uwanja huu ulijaa umati kushuhudia wanaofuzu. Kujaa kwa uwanja huu wa Biko Square ni ishara ya kuwa jamii ya *Maisha Kitendawili* ilithamini elimu. Sherehe za kufuzu ni halisi katika jamii. Vyuo mbalimbali hasa nchini Kenya huadaa sherehe za kufuzu kwa mahafali kila mwaka.Wanaofuzu hupewa vyeti mbalimbali kulingana na taaluma zao. Katika sherehe hizi mahafali wanawaalika jamaa na marafiki kushuhudia kufuzu kwao. Wale wanaotia fora hupewa zawadi kwa kazi zuri waliofanya.

Mandhari haya ya Chuo cha Mzalendo yanaonyesha mbinu mbalimbali zilizotumika na wanafunzi katika kufanya mitihani yao. Kuna wale waliotumia mijadala kabla ya mtihani. Wahusika hawa ni pamoja na Rose, Juma na Amos. Walishirikiana pamoja na kujadili mada tofauti tofauti. Kuna wale ambao walitumia mbinu za mkato ili waweze kufaulu mitihani yao. Mbinu hizi za mkato ni: wanafunzi kuwa katika makundi ya watu watatu watatu, kusoma mada fulani na wakati wa mtihani wanabadilisha karatasi na kunukuu majibu. Wengine waliandika nambari kwenye karatasi bila kuandika chochote na baada ya mtihani wanaondoka na karatasi ili mwalimu, kusimamia mtihani ajibu swali la karatasi ya mwanafunzi. Mbinu nyingine ni kuwa asubuhi yake ya mtihani wangeandika kwenye mapaja majibu ya maswali wanayodhania yangekuwa kwenye mtihani (uk 51). Mandhari haya ya chuoni yanafanikisha ujumbe wa udanganyifu katika mtihani. John Habwe pia ametumia mandhari ya chuoni kuthibitisha uozo unaofanyika chuoni kwa ajili ya wanafunzi kufaulu mitihani. Mwandishi anatumia mhusika Farida kufanikisha uozo huo. Farida anaeleza hawezi kuanguka mtihani wa "supplementary" kwa kuwa anayesahihisha ni mwalimu Manoah na watazungumza kabla ya mtihani (uk.52). Jambo hili la mwalimu Manoah kuzungumza kwanza na Farida kabla ya mtihani ni ishara ya udanganyifu wa elimu unaotendeka chuoni.

Mambo yaya haya ya udanganyifu wa mitihani ni halisi katika jamii, kwani yanadhihirika katika shule mbalimbali na vyuo. Kila mwaka katika nchi ya Kenya visa vya udanganyifu wa mtihani wa kitaifa huripotiwa. Pia udanganyifu huu unadhihirika katika idara mbalimbali za serikali. Watu wanaajiriwa kazi kwa kutumia vyeti gushi na wengine wanapata kazi bila kupata elimu ya kutosha kwa kazi wanazofanya. Wanapopata kazi hizo wanashindwa kuzitekeleza ipasavyo kwani hawana taaluma ya kutosha.

Mwandishi John Habwe ametumia mandhari halisi ya chuoni kudhihirisha uozo unaotendeka chuoni wa udanganyifu wa mtihani. Hata hivyo, mwandishi ametumia mandhari ya chuoni kudhihirisha jamii inayothamini elimu kwa jinsia zote, bila ubaguzi.

**Mandhari ya Kanisani**

Mwandishi ametumia mandhari ya kanisani kuonyesha unafiki unaoendelezwa na viongozi wa kidini pamoja na waumini. Habwe kupitia riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mhusika Rose kuonyesha mtu mnafiki. Mandhari haya ya kanisani yanadhihirisha tabia halisi kuhusu mhusika Rose. "Siku ya Jumapili Rose aliingia kanisani akapiga magoti, akaanza kusali na kutikisa kichwa kama ambaye amebarikiwa na kipawa cha utambuzi Roho Mtakatifu" (uk.56). Rose anapoingia kanisani anajitambulisha kama mtu anayetii amri za Mungu, ilhali yeye ni mtu anayeshiriki usherati na uavyaji mimba. Mwandishi anatudokezea kuwa Rose tayari ametungwa mimba mara nne na kuwatupa watoto pipani. Pia Rose akiwa kanisani anadai kuwa Yesu ameshinda matendo maovu kama uchawi, umalaya, mauti, wizi, uchoyo na uongo (uk. 50). Matendo haya, mhusika Rose aliyatenda na yalikuwa kinyume cha amri za Mungu zinazosema: Biblia; Kutoka (20:13-17) inasema usiue, usizini, usiibe na usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako.

Mandhari haya ni halisi katika jamii kwa kuwa vyumba vya kuabudu vimetumika kama

maficho ya watenda maovu. Kila Jumapili vyumba vya kuabudu huwa vimejaa waumini. Waumini hao kila mmoja huwa na lengo lake la kuhudhuria ibada. Kuna wale wenye nia ya kutubu dhambi zao, wengine wanatafuta baraka za Mungu na wengine wanatumia vyumba hivi vya kuabudu kama maficho yao baada ya kutenda maovu. Wanaotumia kama maficho yao hujiuga na vikundi mbalimbali kama vya waimbaji, vya wanawake au vya wanaume na kuwa na ushawishi mkubwa katika vikundi hivyo. Wengine huteuliwa kama viongozi wa vikundi hivyo kwa kuonekana wema bali ni watu waliojaa hila na dhambi. Vitendo wanavyotenda katikati ya juma huwa vya kutisha lakini siku ya Jumapili wao hudai ni safi kama pamba.

Mandhari ya kanisani pia yamedhihirika katika kanisa la Msalaba Mweusi. Kupitia wahusika Kasu, Mjomba na Farida mwandishi anadhibitisha halisi ya kanisa hili. Mwandishi ametumia kanisa hili kijazanda. Jina Msalaba Mweusi linaonyesha kuwa mambo yaliyotendwa katika kanisa hilo ni kinyume na amri za Mungu. Mandhari haya ya kanisa yanatisha Farida. Hali ya Kanisa hili la Msalaba Mweusi lilikuwa mbaya. "Watu wanaweza kuona ndani wakiwa nje, mlangoni kuna kinyesi cha mbwa. Pia mlango wenyewe unafunguka kwa shida kwa kuwa lenyewe limeinama upande mmoja. Viambaza vya kanisa vimedondoka udongo wake" (uk.130). Hali hii inadhihirisha unafiki wa viongozi wa kanisa. Kiongozi wa kanisa la Msalaba Mweusi badala ya kulikarabati kanisa liwe katika hali nzuri, anafuja pesa za waumini. Kanisa la Msalaba Mweusi licha ya kuwa katika hali mbaya, mwandishi anaonyesha limekuwa kimbilio la wengi. Kila mmoja katika jamii ile anayekumbana na shida awe tajiri au maskini anakimbilia kwenya kanisa hilo na kupata suluhu. Mandhari haya nidhihirisho kuwa kanisa linatumiwa kama maficho ya wanaotenda maovu.

Mandhari haya yamethibitisha hali halisi ya jamii. Makanisa yametumika kama vyumba vya kufanyia biashara na viongozi kuwatapeli waumini wao. Katika bara la Afrika hasa Kenya chimbuko la makanisa limekuwa kwa kiwango kikubwa. Kila ananyefungua kanisa lake ana nia ya kupata waumini zaidi. Kwa hivyo, lazima watumie mbinu mbalimbali za kuwavutia waumini kama, wanadai kuwa na uwezo wa kuponya magonjwa hatari, uwezo wa kuponya walemavu na pia wanaweza kutatua shida mbalimbali zinazokumba wanajamii. Zaidi ya hayo, wanatumia waumini hao kushuhudia kuwa walikuwa na tatizo fulani ila wakaponywa baada ya kuombewa na kupewa mafuta. Mambo haya yamesababisha waumini kutapeliwa mali yao kwa ahadi sisizo za ukweli. Mandhari ya kanisani yalikuwa muhimu kwa mwandishi John Habwe kufanikisha ujumbe wa unafiki wa dini katika jamii.

**Madhari ya Hospitalini**

Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari ya hospitalini kudhihirisha hali halisi ya hospitalini. Hospitali za jamii ya mwandishi zinakumbwa na matatizo kadha wa kadha. Wahudumu wa hospitali kufika wamechelewa, ukosefu wa dawa, utepetevu wa madktari na wauguzi na mazingira machafu ya hospitali.

Mwandishi amedhihirisha haya kupitia mhusika Bwana Omar. Kibibi na mumewe Omar wanafika hospitalini kutafuta matibabu na kupata wahudumu wa hospitali wamechelewa kufika kazini. Kwa hivyo, ilibidi wakae kwenye ubao uliokuwa unatumika kama kiti pale hospialini. Polepole wagonjwa walianza kufika kwa ajili ya kupata matibabu na ubao uliotumika kama kiti ukajaa. Wagonjwa waliofika baada ya ubao kujaa walikaa sakafuni licha ya kuwa na matope (uk.35). Mandhari haya yanaonyesha kuwa sakafu haijapigwa deki kwa siku kadhaa. Jambo hili linadhihirisha kuwa utawala wa hospitali haujawajibika.

Halikadhalika, daktari anapofika hakujali kushughulikia kwanza wagonjwa waliozidiwa na ugonjwa. Jambo hili linasababisha mwanamke aliyezidiwa na ugonjwa kufariki kabla ya kupata matibabu. "Mgonjwa huyu anajinyoosha pale sakafuni hadi anaaga dunia. Bila moyo wa utu, daktari anatoka ndani ya ofisi na kumwangalia jinsi alivyonyooka pale chini (uk. 36). Mandhari haya yametumiwa kudhihirisha mateso wanayoyapitia wagonjwa wanapotafuta matibabu hospitalini.

Mandhari haya ya hospitali ni halisi kwa kuwa yanawasilisha mambo halisi yanayodhihirika

katika jamii. Afya kwa kila binadamu ni muhimu katika jamii ila wanajamii wanapitia changamoto nyingi wanapotafuta matibabu hayo hasa katika hospitali za umma. Katika hospitali hizi wagonjwa hawapati dawa wanazohitaji wanalazimika kununua dawa katika maduka ya kibinafsi ambayo yanauza dawa kwa bei ghali. Zaidi ya hayo, huduma mara nyingi katika hospitali hizi huanza kuchelewa baada ya wagonjwa kulalamika au baada ya mgonjwa kuaga dunia. Pia kwa kuwa idadi ya wagonjwa huwa wengi katika hospitali za umma, wengine hupata matibabu wakiwa wamechelewa na kuwa na maumivu zaidi na hata wengine kuaga dunia kwa kusubiri kwa muda mrefu bila kupokea matibabu. Visa mbalimbali vimeripotiwa kuwa wagonjwa wanapotafuta matibabu wanapata matibabu yasiyostahili. Madaktari wanatibu ugonjwa ambao usio uliostahili kutibiwa. Jambo hili linatokana na matokeo ya udanganyifu wa mitihani katika jamii. Madaktari wanapata vyeti gushi bila kuwa na elimu ya kutosha katika taaluma yao. Hili husababisha wagonjwa kupata huduma duni. Wengine hawajali kufanya kazi kwa kuwa lengo lao ni kuwa kila mwisho wa mwezi watapata mshahara wao. Mateso haya husababisha wagonjwa kutafuta matibabu katika hospitali za kibinafsi ambazo bei ya matibabu ni ghali mno.

**Mandhari ya Ugangani**

Mandhari haya yamedhihirika pale ambapo Bwana Omar na mkewe Kibibi walipokata shauri na kumtembelea mganga Kalulu. Mwandishi anaonyesha picha halisi ya mandhari ya mganga Kalulu yalivyokuwa. Kwanza nyumba yake ilikuwa ndogo kwa hivyo ilibidi anayeingia ndani kupiga magoti hadi ndani (uk.37). Kwenye mlango kulikuwa na maua ya kila aina. Ndani mlikuwa na chupa za kijani, nyekundu, nyeupe zenye midomo mipana na miembamba. Vibuyu vilining'inia ukutani. Kwenye meza kulikuwa na fuvu la kichwa cha mtu. Mganga Kalulu anapomuhudumia Bwana Omar, anamshauri kutia pesa kwenye kibuyu kisha mwenyewe kukizungusha. Familia hii inatapeliwa kiuchumi na kuhangaishwa kutafuta vitu ambavyo mganga alidai. Bwana Omar alikuwa wa tabaka la chini kwa hivyo hakuwa na uwezo wa kupata vitu vilivyotatikana na mganga Kalulu.

Mwandishi ametumia mandhari haya kuwasilisha ujumbe wa ushirikiana na ulaghai. Mandhari haya ya ugangani yanathibitisha jinsi jamii ya mwandishi ililaghaiwa bila kupata suluhu ya matatizo yao. Pia mandhari haya yanadhihirisha jinsi jamii hii iliamini matendo ya ushirikina na kuwa na ukosefu wa elimu na maendeleo.

Mandhari haya ya ugangani ni halisi kwani yanadhihirika katika jamii ya mhakiki. Mabango mbalimbali yamewekwa katika barabara za miji yakitangaza mambo ambayo waganga wanayatatua. Pia kwenye mabango hayo kuna nambari za simu ambazo hutumiwa kwa mawasiliano iwapo unahitaji huduma zao. Katika jamii suala la imani potofu linadhihirika pale wanajamii wanapougua hukimbilia kwa waganga wa jadi badala ya kutafuta matibabu hospitalini. Vyombo vya habari vya nchi za Afrika Mashariki kila mara utangaza kuwa wananchi mbalimbali walitapeliwa baada ya kutafuta usaidizi kwa waganga.

**Mandhari ya Mjini**

Mwandishi ametumia mandhari ya mji wa Soweto. Kupitia mhusika Kasu na Yasmini, mwandishi anadhihirisha halisi ya mji wa Soweto. Katika mji huo wa Soweto mambo kadhaa yanatendeka. Kasu na Yasmini wanafanya biashara ya ukahaba ili wapate pesa za kulipa kodi. Watu wanaoishi katika mji huu hawaishi vituko. Katika mji huu vitendo vya kuavya mimba ni jambo la kawaida. Yasmini anapomwelezea Kasu kuhusu jibwa lililobeba kipande cha mtoto, Kasu anasema haya: "…leo mtu ana mimba kesho hana. Hana mtoto. Yuko wapi? Hana. Mara yuko pipani analiwa na mbwa… "(uk.28). Familia kupigana, watu kuomba kwa kelele ni jambo la kawaida katika mji huu. Mwandishi wa *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari haya kudhihirisha ufukara unaowaathiri wanaoishi mji wa Soweto. Mwandishi ametumia mandhari haya ya mji wa Soweto kufanikisha ujumbe wa utabaka unaodhihirika wazi katika makao ya mijini. Watu wanaoishi katika miji ya mabanda ni watu wa tabaka la chini. Wanaoishi katika miji hii wanapitia changamoto nyingi kama ukosefu wa ajira, ukosefu wa vyumba

vya kulala, mazingira machafu na pia ukosefu wa usalama. Wenyeji wa mabanda hutumia kila njia ili waweze kutimiza mahitaji ya kila siku.

Mandhari haya ya mji wa Soweto pia yametumika kufanikisha ujumbe wa utamaduni. Mwandishi anatumia kundi la Wagisu kutambua utamaduni unaoendelezwa katika mji huo. Kutokana na mandhari haya tunaambiwa: Midundo ya ngoma iliyosikika kwa mbali ilianza kukaribia. Licha ya ngoma kulisikika manyanga na kayamba vilevile. Mara kundi la watu lilitokezea likibenua kwa mabega, viungo, shingo na viungo. Walikuwa wakicheza uchi na ulikuwa huwezi kuwatambua. Mikononi mwao walikuwa na fimbo. Hapa Soweto kuna watu waasili tofauti. Kila kundi linafanya mambo kulingana na mila yake. Hili hapa ni kundi la Wagisu ambalo linatayarisha vijana kwa tohara" (uk. 30).

Dondoo hili linafafanua jinsi jamii ya Wagisu iliendeleza utamaduni wao katika mandhari ya mji wa Soweto. Jambo hili linadhihirisha mila na tamaduni za jamii ambazo zilidumishwa katika jamii ya mwandishi. Bila mandhari haya ya mjini labda ingekuwa vigumu kwa mwandishi kufanikisha ujumbe wa utamaduni. Ujumbe huu wa mila na tamaduni za jamii ni halisi katika jamii. Katika jamii nyingi za bara la Afrika zinadumisha mila na tamaduni mbalimbali kama kupashwa tohara kwa wavulana, ulipaji mahari na pia jinsi ya kuwapa majina watoto wanapozaliwa. Tamaduni hizi zimedumishwa kwa kuwa jamii inachukulia kuwa muhimu na husaidia kizazi kipya kuelewa mila na tamaduni zao.

**Mandhari ya Hali**

Mandhari ya hali huonyesha namna jambo au shughuli ilifanyia. Hali hizi zinaweza kuwa za furaha au huzuni. Mwandishi wa riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari ya hali kuonyesha mambo ambayo jamii yake ilikumbana nayo. Hali hizi zinadhihirika katika mandhari haya: mandhari ya mazishini na mandhari ya afya.

**Mandhari ya Mazishini**

Mwandishi John Habwe ametumia mandhari ya mazishi ya wahusika wake kuonyesha hali ambazo wanajamii walipitia. Mandhari haya yalidhihirika katika mazishi ya marehemu Bwana Omar na Bi. Kibibi. Kibibi aliomboleza usiku na mchana, mkojo ulimtoka ovyo, makamasi yalining'inia na kujigaragaza chini kama wazimu (uk. 40). Kupitia vitendo hivi ni dhahiri kuwa Kibibi alikuwa katika hali ya huzuni.

Halikadhalika, mhusika Kibibi anaomboleza hadi anafariki. Jambo hili linasababisha jamii kutembea mji mzima kwa huzuni. Jambo hili linadhihirisha kuwa jamii ya mwandishi ilishirikiana wakati wa huzuni. Jamii ya Bwana Omar na Kibibi ilitayarisha mazishi ya wapendwa wao. Matanga yalikamilika kwa mazishi ya Bwana Omar na Kibibi. Mwandishi anadokeza kuwa siku ya mazishi, Chifu wa Lokesheni ya Mwasoko alipewa nafasi ya kuhutubia watu waliokuwa wamefika mazishini. Ilikuwa si kawaida watu wa namna hii kuzungumza katika mazishi kwa kuwa wengi walidai ilikuwa ni kuhitilafiana na utaratibu wa kiitikadi (uk. 41).

Mwandishi ametumia mandhari haya ya mazishini kwa Bwana Omar na Kibibi kufanikisha ujumbe wa udumishaji wa mila na tamaduni za jamii ambazo zilistahili kufuatwa. Bila mandhari haya, ujumbe wa kuhifadhi mila haungetambulika.

Mandhari ya hali pia yanadhihirika katika chumba cha kuhifadhi wafu. Mandhari haya ya mochari yalijitokeza pale ambapo Farida aliombwa na jirani yake kuandamana naye ili kuuchukua mwili wa marehemu Julia. Familia hiyo ilikuwa katika hali ya majonzi ila wanakumbana na mambo ya kuogofya. Ufuoni kulikuwa na uvundo wa harufu na kulikuwa na mvuke wa damu mbichi iliyotanda kila mahali (uk .153). Miili ya wafu ilitapakaa kila mahali kwenye sakafu. Zaidi ya hayo, familia ya marehemu Julia inapewa mwili wa marehemu na wahudumu wa mochari baada ya kutoa hongo. Kupitia mandhari haya mwandishi amefanikiwa kuwasilisha ujumbe wa ufisadi. Pia anathibitisha kuwa wahudumu wa ufuoni wamezembea katika kazi yao. Ujumbe huu ni halisi katika jamii kwa kuwa ufuo za umma hapa nchini Kenya zinatoa uvundo ambao unaonyesha kuwa wafanyakazi katika fuo hizo

wamezembea kazini. Zaidi ya hayo, wahudumu hao kila mara hudai hongo ili waweze kuhifadhi miili ya wafu vizuri. Jambo hili limesababisha watu kupeleka wapendwa wao katika mochari za kibinafsi licha ya kuwa ghali.

**Mandhari ya Afya**

Mwandishi anaeleza hali ya afya ya jamii mashambani. Kupitia wahusika mbalimbali mwandishi amedhihirisha hali walizopitia wanajamii katika kuwatunza wagonjwa wao. Familia ya Bwana Omar ilikuwa imezoea hali ya ugonjwa wa pumu. Mwandishi anaeleza kuwa Bwana Omar alizaliwa akiugua ugonjwa wa pumu. Hali hii ilisababisha Bwana Omar kubatizwa majina mbalimbali kutokana na uwele huo (uk. 32). Hali hii ilimfanya mkewe Bwana Omar kuchukuwa jukumu la kumtunza mumewe. Kibibi alifanya kila jitihada kumwangaliana kumshughulikia mumewe. Pia Kibibi ndiye aliyetunza wanawe Farida na Kasu.

Familia ya Mama Josii ni familia nyingine ambayo inajizatiti kutunza familia licha ya bwanake kuwa mgonjwa kwa miaka saba. Mama Josii alijitwika jukumu la kumtuza mumewe na pia watoto wake ambao walikuwa wengi (uk. 68). Ingawa familia hii iliishi katika nyumba iliyovuja ukutani na paani, Mama Josii alihakikisha kuwa mumewe na watoto wake wamepata chakua cha kila siku.

Kutokana na mifano hiyo, inadhihirika kwamba jamii ya mwandishi ilipitia hali mbalimbali. Mandhari ya afya hivyo yalitumiwa na mwandishi kufanikisha ujumbe wa uvumilivu katika ndoa na nafasi ya mwanamke katika jamii. Familia ya Bwana Omar na familia ya Mama Josii zilipitia changamoto nyingi ila wanandoa hao wanadhihirisha uvumilivu. Changamoto hizi ni pamoja na kuyatibu magonjwa ya waume wao, kuwatunza, kutafutia familia lishe bora na kuwapeleka wana wao shuleni. Pia mwandishi ametumia mandhari haya kudhihirisha kubadilika kwa utamaduni wa Kiafrika, kuhusu majukumu ya kulea familia. Jukumu la kuitunza familia mara nyingi huachiwa mwanamume. Mwandishi John Habwe ametumia wahusika wa kike kudhihirisha kubadilika kwa majukumu hayo, na kuonyesha nafasi ya mwanamke katika jamii.

**Hitimisho**

Makala hii imeeleza matumizi ya mandhari mbalimbali katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. Pia yamejadili namna mandhari yanavyochangia katika kufanikisha ujumbe wa mwandishi. Mandhari kama sehemu ambapo matukio ya hadithi hutokea huweza kumpa mwandishi uwezo wa kujenga ujumbe aliokusudia. John Habwe katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia mandhari halisi ambayo yanaonekana katika ulimwengu halisi. Mandhari hayoni kama: mandhari ya nyumbani, mandhari ya chuoni, mandhari ya kanisani, mandhari ya mjini, mandhari ya hospitalini na mandhari ya mazishini.
Mandhari haya yametumika kufanikisha jumbe tofauti tofauti. Mandhari ya nyumbani yanafanikisha ujumbe wa jamii kuundwa na matabaka. Matabaka haya yanadhihirika katika makundi mawili, tabaka la matajiri na tabaka la maskini. Matabaka haya yanadhihirika kupitia mandhari ya nyumbani. Mwandishi anasawiri maisha ya wahusika mbalimbali. Pia, amemchorea msomaji mandhari ya chuoni ili ayatumie makusudi kueleza aina ya uozo unaotukia huko. Aidha, anaeleza ujumbe wa thamani na umuhimu wa elimu kwa kila mtu bila kubagua jinsia. Hali hii inaoana na uhalisia wa baadhi ya jamii za Kiafrika. Mfano wa nchi hizo ni Kenya ambayo ndiyo nchi ya mwandishi. Nchini Kenya elimu ni haki ya kikatiba kwa kila mwananchi. Uozo huo ni pamoja na udanganyifu wa mitihani na ufisadi katika idara mbalimbali za serikali. Mandhari hayo yamethibitisha hali halisi ya yale yanayotendeka chuoni. Mandhari ya kanisani yametumika kufanikisha ujumbe wa unafiki unaoendeshwa na viongozi wa kanisa na pia waumini. Mwandishi ameonyesha picha halisi ya yale yanayotendeka kanisani na jinsi kanisa limetumika kama maficho kwa wanaotenda maovu. Mandhari ya hospitali yametumika kuonyesha mateso wanayoyapitia wagonjwa wanapotafuta matibabu. Mwandishi ametumia mandhari hayo kudhihirisha jinsi utawala wa hospitali ulivyokosa uwajibikaji. Jambo hili si ngeni katika nchi za Afrika ambako wagonjwa wengi hufa kifo wasichostahili kupitia upuuzi wa wahudumu wa afya. Mandhari

ya ugangani yametumika na mwandishi kueleza ujumbe wa ushirikina na ulaghai unoendelezwa na waganga katika jamii. Zaidi ya hayo mwandishi ametumia mandhari ya mazishini na mandhari ya afya kufanikisha ujumbe wa hali wanazopitia wanajamii, utamaduni unodumishwa katika jamii, ushirikiano wa wanajamii na nafasi ya mwanamke katika jamii.

Hivyo basi, mwandishi John Habwe katika riwaya ya *Maisha Kitendawili* ametumia kipengele cha mandhari kwa namna inayostahiki ili kumwezesha kupitisha ujumbe wake kwa njia yenye mnato na kuathiri uelewa wa msomaji. Mandhari halisi yametumika katika riwaya *Maisha Kitendawili* na yanadhihirisha halisi halisi zinazopitiwa na jamii.

**Funding:** This research received no external funding.

**Acknowledgments:** I acknowledge the diverse support offered by the Ministry of Education in Machakos town sub-county.

**Conflicts of Interest:** The author declared no conflict of interest.

**Disclaimer Statement**
This article is part of my on-going M.A studies at the Department of Linguistics and Languages, Machakos University.

**Authors Bionotes**
Shadrack Tete Muia holds a Bachelor of Education Arts degree in Kiswahili and is currently pursuing Master of Arts in Kiswahili at Machakos University, Kenya. His research interests are in Kiswahili Fasihi. John Mutua teaches Kiswahili and serves as the current chair, Department of Linguistics and Languages, Machakos University. Vifo Makoti is a senior lecturer and teaches Kiswahili and translation studies at Machakos University.

**Marejeleo**

Habwe, J. (2000). *Maisha Kitendawili* . Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East Africa Education Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (2008) *Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi. Vide Mulwa Publishers Ltd.

Njogu, K., & Wafula, R. M. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

The Bible Societies (1971). *The Holy Bible*. New York: Collins Bible.

Wamitila, K. W (2008) *Misingi ya Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Mulwa Publishers Ltd.